

Lugha na Mukstadha wa Matumizi yake katika Sekta ya Kilimo Nchini Tanzania

Peter Masanja
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Ikisiri

Mlolongo wa nyaraka za serikali, matamko na kauli za wanasiasa zinataja baadhi tu ya maeneo mahususi ya matumizi ya lugha Nchini Tanzania. Miongozo hiyo inaonekana kuisitiza zaidi hasa matumizi ya lugha katika mfumo wa elimu na mafunzo. Maeneo mengine ya utoaji wa huduma za jamii ikiwamo kilimo hayajapata kutolewa maelekezo kuhusu matumizi ya lugha. Matokeo yake ni vigumu kufahamu lugha gani inatumika katika mukstadha upi wa utoaji wa huduma za kilimo. Hivyo, utafiti huu umechunguza lugha zinazotumika na mukstadha wa matumizi yake katika sekta ya kilimo mkoani Morogoro nchini Tanzania. Kwa kutumia mbinu za hojaji, usaili na uchambuzi wa nyaraka, data zilikusanywa kutoka kwa wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo na katika matini za utoaji wa huduma za kilimo. Uchambuzi wa data umeongozwa na Nadharia ya Ufanyaji Uamuzi ya Eastman (1983). Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kwamba sekta ya kilimo inatawaliwa na hali ya wingilugha. Lugha zilizobainika kutumiwa katika utoaji wa huduma za kilimo ni Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa, Kihispaniola, Kiluguru, Kipogoro, Kikagulu, Kinguu, na Kisagara. Hata hivyo, uwiano wa matumizi ya lugha hizo unatofautiana. Zipo lugha zinazotumika kwa kiwango cha juu na zingine kwa kiwango cha chini. Katika mukstadha wa mashamba darasa lugha ya Kiswahili inatawala ilhali katika mukstadha wa maduka ya pembejeo za kilimo na mfumo wa elimu na mafunzo, Kiingereza ndicho kinachotawala. Kwa hiyo, utafiti huu umehitimisha kuwa kuna haja ya kuwa na sera itakayoongoza matumizi ya lugha katika utoaji wa huduma za kilimo nchini Tanzania.

Maneno Msingi: *Wingilugha, Lugha za Jamii, Uchanganyaji Lugha, Sera ya Lugha*

Utangulizi

Kutokana na umuhimu wa sekta ya kilimo nchini Tanzania, ipo haja ya kuwa na nyenzo za mawasiliano zinazoweza upataji wa taarifa na maarifa sahihi kwa wakulima na wafugaji. Kimsingi kilimo ni sekta ya umma inayohusisha watu kutoka jamii mbalimbali wenye usuli tofauti wa lugha. Hali hii inatokana na kwamba Tanzania ni nchi yenye wingilugha ambapo kuna lugha za jamii, Kiswahili, na lugha za kigeni¹ (Batibo, 1992; Roy-Campbell na Qorro, 1997; MLUTA, 2009; Mekacha, 2011; Msanjila na wenzie, 2011; Simons na Fennig, 2017). Katika hali kama hiyo ya wingilugha, aghalabu huhitajika kuteua na kutumia lugha mojawapo miongoni mwa zilizopo. Endapo hakuna upangaji lugha uliofanyika, ni vigumu kujua lugha ipi inatumika katika mukstadha gani wa matumizi ya lugha. Hivyo basi, utafiti huu umemakinikia lugha na mukstadha wa matumizi yake katika utoaji wa huduma za kilimo nchini Tanzania. Uchunguzi huu umechagizwa na suala la kukosekana kwa sera halisi na changamoto za sera ya kiishara ya Tanzania (Msanjila, 2009; Mekacha, 2011).

Tafiti Mbalimbali Kuhusiana na Sera ya Lugha

Wataalamu mbalimbali wa isimujamii wanaelekea kukubaliana na fasili ya Kaplan na Baldauf (1997) kuwa Sera ya lugha ni jumla ya mawazo, sheria, taratibu, kanuni na utekelezaji wa mabadiliko ya lugha yaliyokusudiwa kufikiwa katika kikundi au jamii (taz. Rubin na Jernudd, 1971; Shohamy, 2006; Msanjila, 2009; Mekacha, 2011; Spolsky, 2012; Trudell na Piper, 2014). Sera za lugha zimegawiwa

¹ Lugha za kigeni ni lugha tofauti na lugha mama zilizopo katika mazingira ambayo hazitumiwi kwa mawasiliano katika nyanja mbalimbali, (taz. Kidami, 2017).

katika makundi mawili yaani, sera halisi na sera za kiishara (Kaplan na Baldauf, 1997). Massamba (2007) na Hans (2017a) wanaeleza kuwa matumizi ya lugha nchini Tanzania yanaongozwa na sera ya kiishara ambayo inatokana na matamko, kauli na nyaraka mbalimbali za viongozi wa serikali. Hii ina maana kuwa Tanzania haina 'sera halisi' inayoongoza matumizi ya lugha (taz. Mekacha, 2011:188; Rugemalira, 2013). Hans (2017) anasema kwamba matamko, kauli na nyaraka za viongozi wa serikali kuhusu matumizi ya lugha nchini Tanzania yameweka msisitizo wa viwango tofauti vya miongozo ya matumizi ya rasilimali lugha zilizopo. Katika mazingira hayo, imekuwa ni nadra sana kwa sera hii kukidhi maeneo yote ya matumizi ya lugha. Hivyo, hutokea sera za namna hii kutogusa baadhi ya maeneo ya matumizi ya lugha (taz. Mekacha, 2011:189). Kwa mfano, nchini Tanzania, sera ya lugha inayodaiwa na Msanjila (2009) kuwamo ndani ya *Sera ya Utamaduni* ya mwaka 1997; inatamka wazi wazi matumizi ya lugha katika sekta ya elimu na mafunzo peke yake bila kuweka bayana matumizi ya lugha katika maeneo mengine ya utoaji wa huduma za jamii. Matokeo yake, maeneo ya huduma nyingine za kijamii kama vile afya, utalii, kilimo na nyinginezo yanakosa kuwa na miongozo kuhusiana na matumizi ya lugha.

Kwa jumla, kama anavyodai Mekacha (2011), kukosekana kwa sera halisi ya lugha, sera za kiishara kutozingatia baadhi ya maeneo ya utoaji wa huduma za jamii huchochea lugha kutumika kwa kuchanganywa au kuingiliana katika sekta za utoaji wa huduma za jamii. Ikumbukwe, sekta za utoaji wa huduma za jamii haziwezi kuepuka kuhusishwa na matumizi ya lugha kwa sababu zinagusa watu wa kada mbalimbali wanaowasiliana ili kutimiza majukumu yao. Sekta ya utoaji wa huduma za kilimo ni miongoni mwa sekta za jamii inayohusisha watu mbalimbali. Mathalani, wapo wakufunzi na wahadhiri wanaofundisha maofisa ugani ambao nao huwaongoza na kuwaelekeza wakulima kwenye shughuli za kilimo. Pia, wapo wafanyabiashara ambao huwauzia wakulima pembejeo na zana mbalimbali za kilimo. Hawa wote bila kuwa na sera thabiti ya lugha itakayowawezesha kuwasiliana kwa lugha faafu inayosawiri utamaduni, ufahamu na jinsi watu wanavyofasiri ulimwengu wao wa kijamii, kiuchumi na kisiasa, maendeleo ya jamii husika yatakwama. Hivyo, sekta mbalimbali za utoaji wa huduma za kilimo nchini Tanzania hazina budi kuwa na miongozo thabiti ya kiseru ya matumizi ya lugha.

Tafiti kadhaa kuhusu matumizi ya lugha katika muktadha wa utoaji wa huduma za kilimo zimefanyika katika nchi mbalimbali. Matokeo yanaonesha kwamba lugha za kigeni zisizo na uamilifu mkubwa katika jamii zinatumiwa katika sekta ya utoaji wa huduma za kilimo (taz. Oladele, 2006; Ngowa na Ryanga, 2011; Matalu, 2013; Mary, 2015). Zaidi ya hayo, wataalamu hawa wamebaini kuwa kuna ukinzani wa lugha zinazotumiwa. Mathalani, lugha zinazotumiwa katika kutolea mafunzo kwa wataalamu wa kilimo zinatofautiana na lugha inayofahamika na wadau wengi wa sekta hii. Kwa ufupi, tafiti zao zinadhihirisha kuwa changamoto za kimawasiliano katika sekta hii zinasababishwa na mapungufu au ukosefu wa miongozo thabiti ya matumizi ya lugha. Katika mazingira ya aina hii, ni vigumu kufahamu ni lugha gani hasa inatumika katika eneo gani la matumizi ya lugha nchini Tanzania. Hivyo, kuna haja ya kuchunguza hali ya matumizi ya lugha katika utoaji wa huduma za kilimo hasa katika maeneo ya jamii zenye wingilugha kama Tanzania.

Ukusanyaji wa Data za Utafiti


Utafiti huu umefanyika mkoani Morogoro hususani wilaya za Morogoro mjini, Mvomero, na Kilosa. Uteuzi wa eneo hili umezingatia sababu mbili. Kwanza, Morogoro ndiyo mkoa unaoongoza kwa uzalishaji wa nyanya, ukiwa unazalisha tani 155,745 kwa mwaka (URT, 2017b). Pili, ufugaji wa wanyama ni miongoni mwa shughuli za kiuchumi katika mkoa huu ambapo ufugaji wa kuku unaongoza kwa idadi inayofikia takribani kuku 431,782 (URT, 2017a). Sampuli ya utafiti ni watoataarifa 78 ambao ni wakulima wa nyanya, wafugaji wa kuku, wahudumu wa maduka ya pembejeo za kilimo, maofisa ugani, wahadhiri na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Data kutoka kwa watoataarifa hawa zilikusanywa kwa hojaji na usaili. Pia, kuna data zilizotokana na matini za utoaji wa huduma za kilimo ambazo ni lebo za vifungashio, vipeperushi, lifleti na mabango ya ukutani. Matini hizi zimetumiwa katika utafiti kutokana na kigezo kuwa zina taarifa zinazohusu lugha zinazotumiwa katika utoaji wa huduma za kilimo.

Nadharia ya Ufanyaji Uamuzi

Nadharia ya Ufanyaji Uamuzi ya Carol Eastman (1983) ambayo ni mwendelezo wa Nadharia ya Upangaji Lugha ndiyo iliyotumiwa katika utafiti huu. Msingi wa nadharia hii ni kwamba upangaji lugha ni kitendo cha kufanya maamuzi mbadala wa matumizi ya lugha. Msingi huu umejengwa katika mihimili miwili. Mosi, ni kuteua lugha miongoni mwa lugha zilizopo katika jamiilugha yenye wingilugha. Pili, kutabiri athari zitokanazo na maamuzi ya uteuzi wa lugha. Hii ina maana kuwa Nadharia ya Ufanyaji uamuzi hujikita katika kutathmini gharama na faida ili kutambua, kupima, na kutathmini athari zinazotokana na uteuzi wa lugha (taz. Thornburn, 1971). Hivyo, kwa kutumia nadharia hii, wapangaji lugha wanaweza kuteua, kutathimini gharama na faida na kutabiri athari zinazotokana na kubadili matumizi ya lugha. Sababu ya kutumia nadharia hii ni kwamba, ni nadharia ambayo imetuongoza katika kubaini lugha zinazotumika kama ni miongoni mwa zilizopo katika jamiilugha ya eneo la utafiti au la. Aidha, kupitia mhimili wa kuteua lugha, utafiti huu utabaini lugha gani zinatumika katika miktadha mbalimbali ya utoaji wa huduma za kilimo katika mazingira ambayo hakujafanyika uamuzi wa kuteua lugha.

Matumizi ya Lugha katika Sekta ya Kilimo

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba katika mkoa wa Morogoro kuna lugha mbalimbali zinazofanikisha mawasiliano baina ya wadau wa kilimo. Hii ina maana kwamba utoaji wa huduma za kilimo katika eneo hili umetawaliwa na hali ya wingilugha. Kuna lugha tisa (9) zilizobainika kutumiwa katika utoaji wa huduma za kilimo kwenye eneo la utafiti. Kielelezo Na 1 kinaonesha kwa muhtasari matumizi ya lugha hizo.




Kielelezo Na. 1: Lugha Zinazotumika katika eneo la utafiti

Chanzo: Uwandani (2021)

Kielelezo Na.1 kinaonesha lugha zinazotumika katika sekta ya utoaji wa huduma za kilimo ni Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa, Kihispaniola na *Lugha za Kijamii*² yaani, Kiluguru, Kipogoro, Kikagulu, Kinguu na Kisagara. Lugha hizo wakati mwingine zimetumiwa peke yake au kwa kuchanganywa. Lugha hizo kimatumizi zimegawanyika katika makundi matatu. Kwanza, lugha moja pekee (Kiswahili au Kiingereza). Pili, mchanganyiko wa lugha mbili (Kiswahili na Kiingereza; Kiswahili na Lugha za Kijamii; na Kiingereza na Kifaransa). Tatu, matumizi ya lugha zaidi ya mbili (Kiswahili, Kiingereza na Lugha za Kijamii; na Kiingereza, Kifaransa na Kihispaniola).

Vilevile, matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa matumizi ya lugha katika eneo la utafiti hayawiani. Kutokana na mchanganuo wa matumizi ya lugha katika utoaji wa huduma za kilimo inaonesha lugha zinatumika kwa viwango mbalimbali. Zipo lugha ambazo zimetumiwa kwa kiwango cha juu ilhali zingine zimetumiwa kwa kiwango cha chini. Kielelezo Na. 2 kinaonesha muhtasari wa uwiano wa matumizi ya lugha katika eneo la utafiti:

² Lugha ya kijamii ni [lugha](#) ambayo ni sehemu ya [utamaduni](#) wa jamii fulani ambao [watu](#) wake wanaiongea kama [lugha mama](#) (Msanjila na wenzie, 2011).



Kielelezo Na. 2: Muhtasari wa Uwiano wa Matumizi ya Lugha

Chanzo: Uwandani (2021)

Kielelezo Na. 2 kinaonesha jinsi lugha katika eneo la utafiti zinavyotumika kwa viwango mbalimbali. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba mchanganyiko kati ya Kiingereza na Kiswahili ndiyo unachukua nafasi ya kwanza kimatuzi ikilinganishwa na lugha nyingine. Lugha hizi zinatumika kwa kiwango cha asilimia 39. Kiingereza kutumiwa sambamba na Kiswahili ni matokeo ya lugha hizo kutumiwa katika kufundishia ngazi mbalimbali za mafunzo nchini Tanzania (WEMU, 2014). Isitoshe, bidhaa nyingi za kilimo zinazouzwa nchini zimetengenezwa nje ya nchi. Hivyo, maandishi ya kufafanua matumizi ya bidhaa husika hutolewa kwa Kiingereza na kupewa fasili yake kwa Kiswahili. Hali hii hupelekea lugha hizi kutumiwa kwa kuchanganywa.

Hata hivyo, watoataarifa waliokiri kumudu kutumia mchanganyiko wa lugha unaohusisha Kiingereza katika sekta hii, wengi wao ni wale wa tabaka la wasomi. Hili ni tabaka lenye maofisa ugani, wahadhiri na wanafunzi wa SUA pamoja na wahudumu wa maduka ya pembejeo za kilimo. Mhalani, kati ya watoataarifa 32 waliokiri kutumia Kiswahili na Kiingereza katika eneo la utafiti, ni mtoataarifa mmoja (1) tu asiyehusishwa na makundi hayo alikiri kumudu mchanganyiko wa lugha hizi. Aidha, Kiingereza kuendelea kutumika sambamba na Kiswahili kwa tabaka hili la wasomi kunachagizwa na kwamba lugha hiyo ndiyo ya kufundishia katika ngazi mbalimbali za mafunzo ya kilimo nchini Tanzania.

Lugha ya Kiswahili pekee inafuatia kimatuzi ambapo imedhihirika kutumiwa kwa kiwango cha asilimia 24.6. Kimsingi, kutawala kwa Kiswahili katika utoaji wa huduma za kilimo kunasababishwa na lugha hii kuwa inaeleweka kwa Watanzania wengi na tena ni lugha ya taifa inayofungamana na utamaduni wa Watanzania. Isitoshe, Kiswahili ni lugha ya kufundishia katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo nchini Tanzania (taz. WEMU, 2014; WEU, 1997). Watanzania takribani 90% wanamudu vyema lugha hii (Mekacha, 2011; Kidami, 2017). Kwa hiyo, ni jambo la kawaida kuona Kiswahili kikitawala katika sekta ya utoaji wa huduma za kilimo mkoani Morogoro.

Lugha hiyo ya Kiswahili imefuatiwa kimatuzi na lugha ya Kiingereza. Kiwango cha matumizi kwa lugha hiyo kimedhihirika kuwa ni 13.6%. Mojawapo ya sababu ya matumizi ya lugha ya Kiingereza katika eneo la utafiti ni pembejeo nyingi kutengenezwa katika nchi zinazotumia lugha husika kama lugha rasmi. Lugha rasmi ya nchi ilipo kampuni mtengenezaji wa bidhaa husika hushajiisha matumizi ya lugha ya kutolea maelekezo. Kwa hiyo, matini andishi za utoaji wa huduma za kilimo zimeandikwa kwa Kiingereza kwa sababu hiyo. Sababu nyingine ni kwamba Kiingereza ndiyo lugha sambazi³ ya ulimwengu. Hivyo, ni jambo la kawaida kwa makampuni ya uzalishaji wa bidhaa za huduma za kilimo kutoka nchi mbalimbali duniani kupendelea kutumia Kiingereza. Wanatumia Kiingereza kutambulisha na kutoa maelezo ya matumizi ya pembejeo za kilimo ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano kiulimwengu.

³ Lugha ambayo ina sifa ya kuvuka mipaka ya kijamii inayotumiwa na makundi ya watu yenye lugha tofauti kwa ajili ya mawasiliano baina yao. Kwa mfano lugha ya Kiswahili katika maeneo ya Afrika Mashariki.

Kundi la lugha linalofuata kimatuzi linahusisha mchanganyiko wa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Lugha za Kijamii. Kundi hili la lugha limejitokeza kwa kiwango cha 10.1%. Nchini Tanzania, lugha hizo za kijamii zinatumiwa na watu wa jamii mbalimbali ambao kwa jumla wanafanya jamiilugha moja pana ya wanaotumia Kiswahili. Katika mkoa wa Morogoro kuna mchanganyiko wa watu wengi kutoka jamii mbalimbali zenye lugha tofautitofauti. Matalani, kuna jamiilugha zinazongumza Kiluguru, Kinyakyusa, Kigogo, Kipogoro, Kimasai, Kikagulu, Kinguu, Kisagara na kadhalika. Hata hivyo, lugha hizo zimetumiwa kwa kiasi kidogo kwa sababu haziwaunganishi watu kutoka katika jamiilugha hizo zinazounda jamiilugha moja pana. Matokeo yake lugha hizo hazipewi nafasi ya juu kimatuzi katika maeneo ya huduma za kijamii kwa kuwa hazigusi umma mpana wa Watanzania.


Halikadhalika, katika eneo la utafiti kuna uchanganyaji lugha unaohusisha Kifaransa na Kiingereza (asilimia 2.5), na Kiingereza, Kifaransa na Kihispaniola (asilimia 0.9). Lugha za Kifaransa na Kihispaniola zimetumiwa kwa kiwango cha chini, kwa kuwa lugha hizi hazina uamilifu mkubwa nchini Tanzania. Hali hii inashabihiana na maelezo katika WEU (1997), kuwa lugha za Kifaransa, Kihispaniola na lugha nyingine za kigeni zinatuzeshwa kuwasiliana na watu wa mataifa mengine na kuendesha shughuli za biashara.

Muktadha wa Matumizi ya Lugha katika Utoaji wa Huduma za Kilimo

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwapo kwa matumizi ya lugha tofauti katika maeneo mbalimbali ya utoaji wa huduma za kilimo. Maeneo hayo ni pamoja na mashamba darasa, maduka ya bidhaa za kilimo, na kwenye taasisi za mafunzo ya kilimo.

Matumizi ya Lugha katika Mashamba Darasa

Shamba darasa ni mahali ambapo kikundi cha wakulima au wafugaji hukutana na kupata mafunzo ya kilimo kwa vitendo chini ya uangalizi wa mtaalamu wa kilimo, aghalabu ofisa ugani. Wadau wa kilimo wanaokutana katika muktadha wa mashamba darasa aghalabu huwa watu wa kutoka jamii mbalimbali wakiwa na usuli tofauti wa lugha. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha katika mashamba darasa kuna wanaozungumza Kiswahili, Kiingereza, Kiluguru, Kikagulu, Kipogoro, Kinguu na Kisagara. Ili kuwa na mawasiliano miongoni mwa wadau hao hakuna budi kuwa na lugha itakayoweza kuwaunganisha wote. Kwa sababu hiyo, lugha inayotawala katika matumizi kwenye eneo hilo huwa ya mawasiliano mapana ambapo nchini Tanzania lugha hiyo ni Kiswahili. Matokeo ya



uchambuzi huo umewasilishwa katika Kielelezo. Na. 3 kama ifuatavyo:

Kielelezo Na. 3: Uwiano wa Matumizi ya Lugha katika Mashamba Darasa

Chanzo: Uwandani (2021)

Kielelezo Na. 3 kinaonesha lugha zinazotumika katika mashamba darasa kuwa ni Kiswahili, Kiingereza na lugha za kijamii. Lugha ya Kiswahili ndiyo lugha inayotumika pekee ilhali lugha nyingine (Kiingereza na Lugha za Kijamii) zinatumiwa kwa kuchanganywa na Kiswahili. Takwimu zinaonesha matumizi ya Kiswahili pekee katika mashamba darasa ni 35.5%. Hii inaonesha Kiswahili kinatumika zaidi ukilinganisha na lugha nyingine. Asilimia 64.5 zilizobaki ni za matumizi ya lugha

mchanganyiko. Hata hivyo, katika matumizi ya lugha mchanganyiko na Kiswahili kimo. Hii ina maanisha kuwa Kiswahili ndiyo lugha kuu ya mawasiliano katika mashamba darasa.

Aidha, kuhusiana na matumizi ya lugha mchanganyiko, uchanganyaji wa Kiswahili na Kiingereza ndio unaotumika zaidi katika mashamba darasa ukilinganisha na mchanganyiko mingine. Kwa kuwa lugha kuu ya mawasiliano kwenye mashamba darasa ni Kiswahili, Kiingereza huchanganywa hapa na pale kwa lengo la kuziba pengo la kiistilahi. Istilahi nyingi za pembejeo za kilimo ni za Kiingereza. Matokeo yake wadau wa kilimo hulazimika kutaja baadhi ya istilahi hizo kwa Kiingereza kwani hukosa istilahi mbadala katika Kiswahili wakati wa mawasiliano. Tazama Kielelezo Na. 4:

GROWERS MASH
(16.2% CRUDE PROTEIN, 2870 Kcal)

Baada ya wiki 6 endelea na Grower Mash. Growers Mash itumike hadi kuku wanataga kwa 5%.

LAYERS MASH
(15.43% PROTEIN, 2675 Kcal)

Endelea na Layers Mash kuku wanapotaga kwa asilimia 5. Kuku wakiwa wametunzwa vizuri wataanza kutaga wakiwa na wastani wa wiki 16 au miezi 4.

ULISHAJI:

Kuku 400 wanakula mfuko Mmoja (1) kwa Layers kwa siku

Kielelezo Na. 4: Kipeperushi chenye mchanganyiko wa lugha

Chanzo: Uwandani (2021)

Katika kielelezo Na. 4 kuna mchanganyiko wa matumizi ya lugha za Kiswahili na Kiingereza. Hata hivyo, lugha ya Kiswahili ndiyo iliyotawala zaidi katika matini hiyo. Kwa maana hiyo, lugha kuu ya mawasiliano katika Kielelezo Na. 4 ni lugha ya Kiswahili. Pamoja na kwamba katika matini hiyo lugha kuu ya mawasiliano ni Kiswahili, bado matini hiyo ina maneno ya Kiingereza kama vile: *growers mash*, *crude protein*, *protein*, *layers mash*, na *layers*. Maneno haya ya Kiingereza yametumiwa kwa kuchanganywa na Kiswahili wakati wa mazungumzo.

Vilevile, katika muktadha wa mashamba darasa kuna matumizi ya lugha za kijamii ambazo hutumiwa sambamba na Kiswahili au Kiswahili na Kiingereza. Kwa kawaida lugha hizi hutumiwa na watu wanaotoka jamii moja wenye usuli sawa wa lugha. Licha ya kuwa katika mashamba darasa hutokea wakakutana na watu kutoka jamii mbalimbali na wenye usuli tofauti wa lugha, bado lugha za kijamii hutumika hasa kwa lengo la kuziba pengo la kimawasiliano. Hali hii hutokea pale anapotokea mdau mmojawapo katika shamba darasa kukosa stadi za kutosha kuwasiliana kwa Kiswahili. Matalani, mtoa taarifa mmojawapo miongoni mwa maofisa ugani alikuwa na haya ya kusema:

...Mara nyingi ninatumia Kiswahili na wakati mwingine kwa kuchanganya na lugha za kikabila pale inapobidi hasa kwa mdau wa kilimo asiyejua vyema lugha ya Kiswahili. Ninafafanua jambo kwa lugha yake (...) kama siujui ninamuomba mkulima mmojawapo anayejua lugha hiyo kusaidia kutoa ufafanuzi. Kwa mfano,

tunachanganya Kiluguru, Kipogoro na lugha nyingine za kikabila...

Chanzo: Uwandani (2021)

Maelezo hayo yanatuonesha kwamba uchanganyaji unaohusisha Lugha za Kijamii hutumika pale mdau wa kilimo anapokosa stadi ya kutosha kuwasiliana kwa Kiswahili au Kiingereza. Hivyo, ofisa ugani ambaye ni mwenyeji wa jamii au anamudu lugha ya mteja wake hulazimika kutumia lugha hiyo kwa kuchanganya na Kiswahili. Aidha, inapotokea ofisa ugani hajui lugha ya mdau, huwashirikisha wadau wengine kumuelimisha mkulima husika kwa lugha yake. Hata hivyo, aghalabu lugha hizi hutumika tu katika kutaja majina ya magonjwa ya mimea, mifugo na mbolea. Baadhi ya istilahi za Kiingereza zilizobainika uwandani ni kama vile *Newcastle Disease* (ugonjwa wa kuku), *water rot* na *funga* (magonjwa ya mimea). Maofisa ugani wanakiri kuwa ni vigumu kuyaeleza magonjwa kama haya mpaka yaeleweke kwa kurejelea majina ya Kiingereza yaliyotumika ama katika kifungashio au matini zingine za kilimo. Kwa hiyo, katika mashamba darasa wataalamu wa kilimo hulazimika kutumia mbinu zao wenyewe ili kuhakikisha kuwa wakulima wameelewa vyema. Mathalani, ofisa ugani mmojawapo alikuwa na haya ya kueleza:

...wakati mwingine tunalazimika kutaja baadhi ya majina ya dawa na magonjwa kwa Kiswahili na lugha za kikabila. Kwa mfano, *Newcastle Disease* ugonjwa unaowapata jamii ya ndege ambao kwa Kiswahili unaitwa *mdondo* au *kideri* ambapo Kipogoro unajulikana kama *mdonde*. Pia, kuna magonjwa mengine kama '*funga*' ambayo kwa Kiswahili tunaita *ukungu* au *kuvu* na Kipogoro *inyala*...**Chanzo:** Uwandani (2021)

Dondoo linaonesha kuwa lugha za kijamii zinatumiwa katika utoaji wa huduma za kilimo kama mbinu ya kutatua changamoto za kiistilahi zinazowakabili wakulima na wafugaji wakati wa kutumia pembejeo za kilimo zenye majina ya Kiingereza. Ingawa lugha za Kijamii ni mojawapo ya lugha zinazounda idadi kubwa ya wazungumzaji wazawa wanaopatikana Tanzania, utafiti huu umebaini kwamba hakuna kundi linalotumia lugha za Kijamii peke yake katika eneo la utafiti. Jambo hili linashabihiana moja kwa moja na maelezo ya Mekacha (2011) kuwa hadi kufikia mwaka 2001 Watanzania karibu wote walikuwa na umilisi wa lugha ya Kiswahili kwa namna moja au nyingine.

Matumizi ya Lugha katika Maduka ya Pembejeo za Kilimo

Kama ilivyo katika muktadha wa mashamba darasa, matokeo ya utafiti yanaonesha pia Kiswahili kikitawala katika mawasiliano baina ya wahudumu wa maduka ya pembejeo za kilimo na wateja wao yaani wakulima na wafugaji. Kwa mfano, mhudumu mmojawapo alipoulizwa kuhusu lugha anayotumia kuwasiliana na wateja katika eneo lake la huduma anasema:

Lugha ambayo ninatumia kuwasiliana na wateja wangu ni Kiswahili kwa maana ni lugha nyepesi ambayo hata mtu ambaye hajaingia darasani anamudu kuitumia kwa namna moja ama nyingine. Ingawa maelezo ya matumizi ya bidhaa nyingi hapa dukani yapo kwa Kiingereza, bado tunatumia Kiswahili kuwaelevesha wateja wetu matumizi ya bidhaa hizo. Unajua tena kuwa wateja wetu wengi hawajui Kiingereza kabisa. Fikiria mtu aliyeishia darasa la saba ni ngumu sana kujua Kiingereza. Hivyo, Kiswahili ndiyo kinabaki kuwa mwarobaini kwetu. **Chanzo:** Uwandani (2021)


Nukuu hiyo inaonesha kwamba, katika muktadha wa maduka ya pembejeo za kilimo lugha ya Kiswahili inatawala zaidi. Mawasiliano baina ya wadau wa shughuli za kilimo mara nyingi yanafanywa kwa lugha hiyo.

Licha ya kwamba bidhaa nyingi zinazouzwa katika maduka hayo zimeandikwa kwa Kiingereza, bado lugha hii haipewi nafasi kubwa katika muktadha wa mawasiliano baina ya wahudumu wa maduka na wateja wao. Lugha hii inapotumika katika mawasiliano madukani hutumiwa kwa kuchanganywa na Kiswahili. Hivyo, katika muktadha wa maduka ya pembejeo za kilimo utoaji wa maarifa na upokeaji hutawaliwa na '*kilugha*' cha kubadili msimbo, ambapo maneno au istilahi za

Kiingereza kuhusu pembejeo huchoppekwa katika miundo ya mazungumzo inayofanyika kwa lugha ya Kiswahili.

Halikadhalika, lugha za kijamii zinatumiwa katika muktadha wa maduka ya pembejeo za kilimo. Jinsi ya matumizi ya lugha hizi katika muktadha huu haitofautiani na ilivyo katika mashamba darasa. Kwa kuwa maduka ya pembejeo za kilimo ni eneo mojawapo la kibiashara ni nadra sana kukuta matumizi ya lugha za kijamii. Kama asemavyo Mekacha (2011) kwamba masoko na biashara za ndani ya Tanzania hutawaliwa na matumizi ya Kiswahili. Kwa sababu hiyo, katika maduka ya pembejeo za kilimo matumizi ya lugha za kijamii ni kidogo.

Pamoja na kwamba mawasiliano baina ya wahudumu wa maduka ya pembejeo za kilimo yanatawaliwa na Kiswahili, hali ni tofauti na ilivyo katika matini andishi. Uchambuzi wa data za utafiti unaonesha matini hizo zinatumiwa zaidi lugha ya Kiingereza. Lugha hii ama inatumika pekee yake au kwa kuchanganywa na lugha nyingine. Kwa mujibu wa utafiti huu, lugha zilizobainika kutumika katika maandishi mbalimbali ya utoaji wa huduma za kilimo ni nne. Kielelezo Na. 5 kinaonesha mtawanyiko wa lugha andishi kwenye maduka ya pembejeo za kilimo.



Kielelezo Na. 5: Lugha Zinazotumika katika Matini Andishi za Sekta ya Kilimo

Chanzo: Uwandani (2021)


Kielelezo Na. 5 kinaonesha lugha zinazotumika katika matini andishi ya sekta ya kilimo ambazo ni Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa, na Kihispaniola. Katika eneo la utafiti kuna matini andishi za lugha moja, mbili au zaidi. Miongoni mwa matini andishi zilizochunguzwa kuna zilizodhihirika kuwa na maandishi ya lugha moja tu. Aidha, kuna matini andishi zinazohusisha matumizi lugha mbili au zaidi katika matini moja. Matokeo ya utafiti yanaonesha matini andishi 22 ni za lugha moja wakati matini 18 ni za lugha zaidi ya moja. Hii ina maana kwamba, katika mawasiliano ya kimaandishi, matini za lugha moja ndiyo zinazotawala katika utoaji wa huduma za kilimo.

Hata hivyo, matini andishi za lugha moja zinapolinganishwa, lugha ya Kiingereza ndiyo inayotumika zaidi kuliko Kiswahili. Pamoja na hayo, lugha ya Kiingereza imetumiwa kwa kuambatanishwa na takribani lugha zote zilizodhihirika kutumika katika utoaji wa huduma za kilimo. Kwa hiyo, lugha hii inatumika pekee au kwa kuchanganywa na lugha zingine kama inavyoonesha katika Kielelezo Na. 5.

Kiwango kikubwa cha matumizi ya lugha ya Kiingereza katika maandishi ya sekta ya kilimo yanachochea na hadhi na nafasi yake kitaifa na kimataifa. Hivyo, si jambo la kustaajabisha kuona bidhaa mbalimbali zinazouzwa katika maduka ya pembejeo za kilimo zimeandikwa kwa lugha hiyo. Hii ni kwa sababu kwamba bidhaa zinazouzwa madukani mara nyingi soko lake linavuka mipaka ya nchi mtengenezaji. Mathalani, mhudumu mmoja wa maduka ya pembejeo za kilimo alikuwa na maoni yafuatayo kuhusu Kiingereza kutawala zaidi kwenye mawasiliano ya kimaandishi:

...matini nyingi za pembejeo za kilimo tunazouza dukani zimeandikwa kwa Kiingereza. Aa! kulingana na nionavyo mimi, hali hii husababishwa na mambo kama mawili hivi. Kwanza, hutegemea na lugha ya nchi mtengenezaji yaani kiwanda cha uzalishaji wa bidhaa hiyo ni wapi. Hivyo, uagizaji wa bidhaa kutoka nje, hufanya bidhaa agizwa kuja na lugha ambayo hutumika huko. Pili, Kiingereza hutumiwa kwa kuwa ndiyo lugha ya dunia kwa sasa. Kwa hiyo makampuni mengi ya uzalishaji wa pembejeo za kilimo hutumia lugha hii kutolea maelezo ya matumizi ya bidhaa zao kwa ajili ya soko la dunia. **Chanzo:** Uwandani (2021).

Maelezo yanayoelezwa katika nukuu hapo juu yanatoa picha kwamba matumizi makubwa ya lugha ya Kiingereza yanatokana na uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Hii ina maana kwamba, pembejeo za kilimo nyingi zinazouzwa huwa zimetengenezwa katika nchi ambazo wanatumia lugha hiyo kama lugha rasmi. Jambo linaloonekana katika ufafanuzi huu ni kwamba lugha rasmi ya nchi ilipo kampuni mmiliki wa bidhaa husika hushajiisha matumizi ya lugha ya kutolea maelekezo ya kutumia. Kwa hiyo, maandishi ya Kiingereza katika matini za utoaji wa huduma za kilimo yanaonesha kuwa bidhaa zinazouzwa zimetengenezwa katika nchi ambazo wanatumia lugha hiyo. Kielelezo Na. 6 kinaonesha mfano wa lifleti ya bidhaa iliyozalishwa nje ya Tanzania iliyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza pekee:



Kielelezo Na. 6: Lifleti ya Bidhaa Iliyozalishwa Nje ya Tanzania

Chanzo: Uwandani (2021).

Kielelezo Na. 6 ni lifleti yenye maelezo ya matumizi ya dawa iliyoandikwa kwa Kiingereza pekee. Kama ambavyo imekwishakuelezwa awali, wakati mwingine lugha ya matini andishi za kilimo hutegemea lugha ya nchi mtengenezaji wa bidhaa. Hivyo, hapa Kiingereza kimetumika kwa sababu bidhaa husika imetengenezwa na kampuni iliyoko nchini India. Matumizi hayo ya Kiingereza yanapewa nguvu na sera ya lugha ya India inayotambua lugha hiyo kama mojawapo ya lugha rasmi (taz. Shil, 2021). Kwa hiyo, bidhaa mbalimbali zilizotengenezwa katika nchi hiyo huandikwa kwa Kiingereza. Matokeo yake bidhaa hiyo inapoingia katika soko la Tanzania huja na maandishi ya lugha hiyo.

Aidha, matokeo ya utafiti yanaonesha hata nchi ambazo hazitumii Kiingereza kama lugha rasmi zimekuwa zikitumia lugha hii. Lengo ni kutambulisha na kueleza bidhaa zao ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano kiulimwengu. Kielelezo Na. 7 kinaonesha maandishi ya Kiingereza kwa bidhaa iliyotengenezwa katika nchi ambayo lugha hiyo si rasmi.

BAOXYTETRA 10%
100mg/ml Oxytetracycline Hcl injection

DESCRIPTION:
Baoxytetra 10% is a sterile solution of Oxytetracycline hydrochloride with antioxidants, complex agents and solvents. Oxytetracycline hydrochloride is a broad spectrum antibiotic with bacteriostatic action against a large number of gram-positive and gram-negative organisms. The bacteriostatic effect is based on the inhibition of the synthesis of bacterial proteins.

COMPOSITION: Each 1ml contains Oxytetracycline hydrochloride (calculated on oxytetracycline) 100mg


INDICATIONS:
For the treatment of bacterial infections diseases caused by gram- positive and gram- negative bacteria affecting respiratory, gastrointestinal tract, Septicaemia as well as mastitis, skin condition and urogenital tract infections, it is also active against mycoplasma, spirochete and some protozoa.

DOSAGE AND ADMINISTRATION: Administered by deep Intramuscular Cattle, Buffaloes, Camel, Sheep, Goats and Pigs:
Single dose 1ml every 10kg b.w by Intramuscular route only. Poultry 1ml/hen Divide the dose and administer at 2-3 different sites.

CONTRA-INDICATION:
1. Baoxytetra 10% is not recommended for use in horses, dogs and cats.
2. Do not administer animals with established hypersensitivity to tetracycline.
3. The use of Baoxytetra 10% during the period of tooth and bone development, including late pregnancy, may lead to discolouration.
4. Do not dilute Baoxytetra 10%
5. If concurrent treatment is administered, use a separate injection site.

CAUTION:
1-Use a dry sterile needle and syringe, do not exceed the above mentioned dosage.
2-Stop medication at least 14 days prior to slaughter of the animals for meat purpose.
3-Milk of treated animals should not be used for human consumption 3 days post administration.
4-Keep out of reach of children.

WITHDRAWAL TIME: Meat: 14 days, milk: 3 days
PACKING: 50ml/glass bottle, 100ml/glass bottle, 250ml/glass bottle, 500ml/glass bottle
STORAGE: Store in cool and dry place and not above 30°C protecting from light. Not freeze. The preparation may darken on exposure to air but the potency of the oxytetracycline remains unchanged. It is better to use it up in one week after opening.

 Manufactured by: Hebei Yuanzheng Pharmaceutical Co., Ltd.
Shizheng Road, Shijiazhuang, Hebei Province, China.

Kielelezo Na. 7: Bidhaa Iliyotengenezwa Nchi ambayo Kiingereza si Lugha Rasmi

Chanzo: Uwandani (2021)

Katika Kielelezo Na. 7 lugha ya Kiingereza imetumiwa katika maandishi ya bidhaa iliyotengenezwa China. Katika nchi hii, lugha ya Kiingereza matumizi yake hayatawaliwi na kanuni na sheria yaani si lugha rasmi ya nchi (Yuming, 2015). Kimsingi, hapa matumizi ya Kiingereza yameegemezwa katika dhana ya umataifa. Hivyo, matumizi ya lugha hiyo yanahusishwa na mikakati ya matumizi ya lugha kibiashara ili kukidhi haja ya soko la dunia. Juhudi za kufikisha taarifa za biashara kwa wateja duniani ambao wana usuli wa lugha tofauti na ya mzalishaji huchangia matumizi ya Kiingereza.

Kundi linalofuata ni mchanganyiko wa Kiswahili na Kiingereza. Matini zilizo zilizoandikwa kwa lugha hizo ni 14. Lugha hizi zinapoandikwa kwa kuchanganywa zinaweza kuainishwa katika makundi mawili. Maandishi ya lugha 'A' kuambatanishwa na tafsiri yake katika lugha 'B' na maandishi ya lugha 'A' kubeba maudhui tofauti na ya lugha 'B'. Katika kundi la kwanza, maandishi huandikwa kwa lugha fulani kisha kuambatanishwa na tafsiri yake katika lugha nyingine moja au zaidi. Kimsingi, tafsiri hiyo hufumbata ujumbe uliopo katika matini chanzi. Hivyo, maudhui ya lugha 'A' huhawilishwa katika lugha 'B'. Kielelezo Na. 8 kinadhihirisha mchanganyiko wa lugha unaosawiri kundi hili:



Kielelezo Na. 8: Kifungashio cha Lugha Mchanganyiko wa Kiswahili na Kiingereza
Chanzo: Uwandani (2021)

Katika Kielelezo Na. 8, lugha ya Kiingereza imetumiwa katika kifungashio sambamba na Kiswahili. Maelezo yaliyotolewa kwa Kiingereza (lugha chanzi) yametafsiriwa katika Kiswahili. Tafsiri ya Kiswahili imebeba maudhui yote ya lugha chanzi. Mathalani, tungo ya Kiingereza 'Fungicide for the control of fungal diseases on horticultural crops and powdery mildew on cashew' imepewa tafsiri yake katika Kiswahili. Tafsiri iliyopewa ni 'Kiuakuvu cha kudhibiti magonjwa ya kuvu kwenye mazao ya mbogamboga, na ubwiriunga kwenye korosho'. Kimsingi, hapa lugha zote mbili zimetumiwa kwa pamoja kufikisha ujumbe ule ule kwa wadau wa kilimo waliolengwa kutumia bidhaa husika. Matumizi ya lugha hizi kwa pamoja yanaashiria kuwa katika eneo la utafiti kuna watu wanaomudu kusoma na kuelewa lugha zote mbili au mojawapo ya lugha hizo. Kwa hiyo, matumizi haya ya lugha yanatoa wigo mpana kwa wadau wa kilimo kusoma na kuelewa maelezo yaliyopo katika bidhaa husika kutegemeana na umilisi wa lugha walionao baina ya lugha zilizotumika.

Pili, matini ambazo zimeandikwa kwa lugha zaidi ya moja huku kila lugha ikiwa imebeba maudhui tofauti na yale ya lugha nyingine. Hii ina maana kwamba maana iliyobebwa na kifungu **A** ni tofauti kabisa na maana iliyomo katika kifungu **B**. Hivyo, lugha hizo hutumiwa kwa kukamilishana katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa mtumiaji wa bidhaa husika. Kwa mfano tazama Kielelezo Na. 9:

S/N	Product	Product code	Packaging	Agent/Wholesaler Price	Consumer/Retail Price	Agent/Wholesaler Margin
1.	Broiler Starter Crumber (BSC)	772	50kg	TZS 40,000	TZS 43,000	TZS 3,000
2.	Broiler Grower Pellet (BGP)	777	50kg	TZS 58,000	TZS 61,000	TZS 3,000
3.	Broiler Finisher Pellet (BFP)	778	50kg	TZS 57,000	TZS 60,000	TZS 3,000

NOTE:
 • Prices are Exclusively for the Dar es salaam & Pwani regions
 • Agent Price 25 bags
 • For Special Offers call: +255 743 366 091

KINAPATIKANA KWA MAWAKALA WOTE

NutriGroup Tanzania Ltd
 25 Mbozi Road,
 Plot 163 Chano omba, P.O Box 45456
 Dar es Salaam, Tanzania

Kielelezo Na. 9: Bango la Lugha Mchanganyiko wa Kiingereza na Kiswahili
Chanzo: Uwandani (2021)

Kielelezo Na. 4.6 kinaonesha bango lililoandikwa kwa lugha mchanganyiko. Sehemu ya juu ya bango hili imeandikwa Kiingereza ‘NutriFeed feed for growth,’ ‘BROILER FEED,’ ‘DAR ES SALAAM PRICE LIST EFFECTIVE FROM 22nd FEBRUARY 2021’, ‘NOTE: Prices are Exclusively for the Dar es salaam & Pwani Regions; Agents Price 20 bags; For special Offers call: +255 743 366 091’. Aidha, katika bango hili kuna maandishi ya Kiswahili ‘KINAPATIKANA KWA MAWAKALA WOTE’. Kimsingi, ujumbe uliotolewa katika vifungu vya Kiingereza havikutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, halikadhalika ule uliotolewa katika kifungu cha Kiswahili hakikuhawilishwa katika Kiingereza. Hivyo, ujumbe uliomo katika vifungu vya Kiingereza ni tofauti na uliomo katika Kiswahili.

Halikadhalika, matokeo ya utafiti yanaonesha katika maduka ya pembejeo za kilimo kuna matini zilizoandikwa kwa Kiswahili pekee. Asilimia 15 ya matini zilizochunguzwa kwenye utafiti huu zimeandikwa kwa lugha hiyo. Kwa mfano, Kielelezo Na. 10 kinaonesha kifungashio cha dawa kilichoandikwa kwa lugha ya Kiswahili pekee:



Kielelezo Na. 10: Kifungashio cha Dawa cha Maandishi ya Kiswahili Pekee

Chanzo: Uwandani (2021)

Kielelezo Na. 10 kina maandishi ya Kiswahili. Lugha hii inapewa nafasi katika sekta ya kilimo kwa sababu Watanzania wengi wanajua kusoma na kuandika kwa Kiswahili (Mekacha, 2011). Hivyo, lugha hii inafahamika na watu wengi kwa kuwa wamepita katika mfumo wa elimu unaotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia. Mtazamo huu unapata mashiko na mtoataarifa mmojawapo wa kundi la wakulima wa nyanya ambaye alikuwa na haya ya kusema kuhusu lugha ya Kiswahili katika eneo la utafiti:

...kusema ukweli Kiswahili ingefaa zaidi kama kingetumika zaidi katika kuandika matini mbalimbali za huduma za kilimo kwa kuwa watu wanaokusudiwa wengi wetu tunajua kusoma na kuandika zaidi kwa Kiswahili. Kwangu mimi ninaona matumizi ya lugha hii yataturahisishia kusoma wenyewe na kuelewa kile kilichoandikwa kwa urahisi zaidi. Hivyo, ninafikiri kama taifa tungeweka nguvu kubwa katika Kiswahili kwa ajili ya kufafanua huduma tunazotoa...

Chanzo: Uwandani (2021)

Maelezo haya yanaonesha hali halisi ya matumizi ya lugha kuwa Watanzania walio wengi wanamudu kusoma na kuandika kwa Kiswahili kuliko lugha zingine. Isitoshe, matumizi hayo ya lugha ya Kiswahili yanasababishwa na hali ya kuwa ndiyo lugha inayotawala katika mawasiliano ya kila siku miongoni mwa wa Tanzania (Syvester, 2011). Lugha hii inawatambulisha Watanzania na jamii pana ya kitaifa. Kwa hiyo, maelezo katika bidhaa mbalimbali zinapoandikwa ili kuzitambulisha na kuzifafanua kwa wateja huandikwa kwa Kiswahili. Lengo likiwa ni kutoa fursa kwa wadau wa kilimo kusoma kwa lugha waliyo na umilisi nayo na kuelewa kwa urahisi zaidi kile kilichoandikwa kuhusu bidhaa zinazouzwa madukani.

Hata hivyo, katika sekta ya utoaji wa huduma za kilimo, imebainika maandishi mchanganyiko wa Kiswahili na Kiingereza ni mengi kuliko ya Kiswahili pekee. Kiswahili pekee kimedhihirika kutumiwa kwa asilimia 15, ilhali matini zilizochanganywa Kiswahili na Kiingereza ni asilimia 35. Kinachotokea ni kwamba, lugha ya Kiswahili inapoandikwa huchanganywa na Kiingereza kidogo. Kwa maana hiyo maandishi ya Kiswahili hutawaliwa na uchanganyaji lugha, ambapo msamiati na virai vya Kiingereza huchopekwa katika miundo ya Kiswahili. Kielelezo Na. 11 kinaonesha kwa muhtasari jinsi miundo ya tungo za Kiswahili inavyochopekwa istilahi za Kiingereza:



Kielelezo Na. 11: Matini ya Kiswahili Iliyochanganywa Maneno ya Kiingereza

Chanzo: Uwandani (2021)

Kielelezo Na. 11 kimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu tungo zake zinatawala matini nzima. Hata hivyo, matini hii imechopekwa maneno ya Kiingereza kwa lengo ama la kutoa ufafanuzi zaidi, kuziba pengo la kimsamiati au kutaja jina la kampuni. Mathalani, Kielelezo hiki kina fungu la maneno ya Kiingereza “ONE - ONE ANIMAL FEED”. Kifungu hiki kinataja jina la kampuni inayozalisha bidhaa husika. Pamoja na kwamba majina ya makampuni yanatambulisha tu kampuni inayohusika na uzalishaji na usambazaji wa bidhaa husika, bado maneno haya tunayahesabu kama ni ya Kiingereza. Hali hii inatokana na kwamba maneno ‘ONE, ANIMAL na FEED’ yanahusishwa moja kwa moja na Kiingereza kwani yana maana mahususi katika lugha hiyo. Maneno haya visawe vyake vya Kiswahili ni: **one** *kv* -moja; **animal** *n* mnyama; **feed** *n* chakula; malisho (taz. TUKI, 2000). Aidha, neno la Kiingereza “PELLETS” ambalo kisawe chake kwa Kiswahili ni “tambitambi” limechopekwa katika matini. Kwa jinsi neno hili lilivyotumika, linaashiria kuwa waandaji wa kipeperushi wanaona kuwa neno hilo la Kiingereza linafahamika zaidi kwa watumiaji. Hivyo, kisawe chake katika Kiswahili kimewekwa katika mabano kwa lengo la kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu istilahi hiyo.

Maandishi ya Kiswahili yanayonadi bidhaa za kilimo huchopekwa maneno ya Kiingereza kuaksi suala la hadhi za lugha nchini Tanzania. Lugha ya Kiingereza inapewa hadhi ya juu kuliko Kiswahili na lugha za asili (taz. Kawonga, 2020; Kidami, 2017; Lusekelo na Alphonse, 2018). Kutokana na hilo, watu hupendelea kuchopeka maneno ya Kiingereza wanapozungumza au kuandika kwa Kiswahili ili kujiweka katika tabaka la wasomi na wenye mafanikio kiuchumi. Hivyo, uchopekaji wa maneno ya Kiingereza katika miundo ya Kiswahili unaonekana kutumiwa kutambulisha biashara.

Matumizi ya lugha katika jozi hizo mbili (Kiswahili pekee; na Kiswahili na Kiingereza) yanatupatia dokezo kwamba Kiswahili ni lugha inayowafikia na kuwaunganisha watu wengi zaidi kuliko lugha zingine. Hoja hii inatokana na kuwa, kati ya matini 40 zilizochunguzwa, matini 20 zimeandikwa ama kwa Kiswahili pekee au kwa Kiswahili na Kiingereza. Hii inamaanisha kuwa jumla ya matini hizo ishirini (20) zina maandishi ya Kiswahili ndani yake. Hiki ni kielelezo

kinachodhihirisha kuwa lugha ya Kiswahili imetumiwa kwa sababu wateja wengi katika maduka ya pembejeo za kilimo wanaelewa lugha hiyo.

Kwa vyovyote vile matumizi haya ya Kiswahili katika maandishi ya sekta ya kilimo yanachagizwa na hali ya lugha ya Tanzania. Kiswahili ni lugha ya Taifa inayofahamika na Watanzania kwa zaidi ya 90% (Brock-Utne, 2000). Aidha, licha ya kwamba nchini Tanzania kuna idadi kubwa ya lugha za kijamii zinazokadiriwa kufikia 150 (taz. Kawonga, 2020; Kidami, 2017), Kiswahili ndiyo lugha pekee ya kitaifa iliyosanifishwa na taratibu za kuiandika zikajulikana (taz. Mekacha, 2011). Hivyo basi, matumizi ya Kiswahili yanatokana na mbinu za kimasoko za makampuni watengenezaji wa pembejeo za kilimo. Lengo likiwa ni kukidhi haja yao ya kibiashara la kuwafikia wateja ambao wengi wao wanajua kusoma na kuandika kwa lugha hii. Jambo hili ndilo linaloshajiisha matini andishi mbalimbali za utoaji wa huduma za kilimo kwenye eneo la utafiti kuandikwa kwa lugha hiyo pekee au kwa kuchanganywa na Kiingereza.

Lugha zingine kama vile Kifaransa na Kihispaniola zimedhihirika kutumiwa katika maduka ya pembejeo za kilimo kwa asilimia kumi10. Lugha hizi zimetumiwa kwa kuambatanishwa na Kiingereza. Matini zenye maandishi mchanganyiko kati ya lugha ya Kiingereza na Kifaransa ni asilimia 7.5, ilhali lugha ya Kiingereza, Kifaransa na Kihispaniola ni asilimia 2.5. Lugha hizi kwa ujumla wake zimetumiwa kwa kiwango kidogo kutokana na kwamba hazina uamilifu mkubwa katika mawasiliano miongoni mwa wa Tanzania. Kwa hiyo, lugha hizo hazitumiwi katika mawasiliano ya kawaida na ya kila siku isipokuwa kwa mawasiliano ya kimataifa. Nchini Tanzania, matumizi ya lugha hizi yanadokeza kuwa bidhaa zinazouzwa zimetengenezwa katika nchi zinazotumia lugha hizo. Kielelezo Na.13 kinaonesha matini ya utoaji wa huduma za kilimo iliyoandikwa kwa mchanganyiko wa Kifaransa na Kiingereza.



**Kielelezo Na. 12: Matini yenye Mchanganyiko wa Kifaransa na Kiingereza
Chanzo: Uwandani (2021)**

Kielelezo Na. 13 ni kifungashio chenye mchanganyiko Kifaransa na Kiingereza zilizopangiliwa kwa safuulalo yaani kuanzia kushoto kwenda kulia. Kwa mujibu wa Kawonga (2020) lugha inayojitokeza katika nafasi ya kwanza kushoto kisafuulalo inaonesha kupewa umuhimu katika matumizi. Hata hivyo, katika utafiti huu lugha inayojitokeza ya kwanza kushoto kisafuulalo ni

kiashiria kwamba bidhaa imetengenezwa katika nchi inayotumia lugha husika. Kwa hiyo, maandishi ya Kifaransa kwenye Kielelezo Na. 13 ni kiashiria kuwa inatengenezwa ama nchini Ufaransa au nchi inayozungumza lugha hiyo. Aidha, tafsiri ya Kiingereza ni kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la nchi zinazozungumza lugha hiyo.

Matini nyingine za utoaji wa huduma za kilimo zimeandikwa kwa lugha tatu yaani Kifaransa, Kihispaniola na Kiingereza. Vielelezo Na. 14 na 15 vinaonesha matini ya utoaji wa huduma za kilimo zenye mchanganyiko huo:



Kielelezo Na. 13: Kifungashio cha Dawa Upande ‘A’ Kiingereza Chanzo: Uwandani (2021)



Kielelezo Na. 14: Kifungashio cha Dawa Upande ‘B’ Kifaransa na Kihispaniola Chanzo: Uwandani (2021)

Vielelezo Na. 14 na 15 vinatokana na matini moja iliyoandikwa kwa lugha tatu. Kielelezo Na. 14 (upande 'A') wa kifungashio hicho umeandikwa kwa lugha moja Kiingereza ilhali Na. 15 (upande 'B') ni Kifaransa na Kihispaniola. Kama ilivyokwisha kuelezwa hapo awali, maandishi ya lugha hizo yanaashiria kuwa bidhaa zinazouzwa sokoni zimetengenezwa nje ya Tanzania. Bidhaa katika Kielelezo Na. 14 na 15 imetengenezwa Uholanzi. Hivyo, maandishi haya yanaashiria kuwa bidhaa imetengenezwa katika nchi inayotumia mojawapo ya lugha hizo au zote. Licha ya Kidachi kuwa lugha rasmi, Kiingereza pia ni mojawapo ya lugha rasmi katika nchi ya Uholanzi hasa katika sehemu ya Visiwa vya Karibiani vinavyojumuisha Visiwa vya Bonaire, Sint Eustatius na Saba (taz. Dijkhoff, 2010). Aidha, inaonesha lugha za Kifaransa na Kihispaniola zimetumika kwa lengo la kukidhi haja ya kibiashara.

Vilevile, matumizi ya lugha zaidi ya moja katika matini hii ni mkakati wa kimasoko wa kampuni husika ili kujimarisha kibiashara sehemu mbalimbali duniani. Makampuni ya kimataifa yanatumia mbinu ya wingilugha kama mkakati wa kibiashara ili kuwafikia wateja wengi ambao wanaumilisi tofautitofauti wa lugha. Katika kuthibitisha hili, mtoataarifa wa kundi la wahudumu wa maduka ya pembejeo za kilimo alikuwa na haya ya kusema:

...kuna bidhaa humu dukani zimeandikwa kwa lugha moja, mbili na zingine zaidi ya mbili. Mimi ninafikiri kuwa na maandishi ya lugha mbili, tatu au zaidi kwenye matini moja sana inatokana na sababu za kibiashara. Hii ni fursa nzuri kwa watumiaji maana mtu anaweza akasoma na kuelewa vizuri kwa lugha yake. Ikiwa wameandika Kiingereza, Mhispaniola hajui kusoma Kiingereza au hapa wameandika Kiswahili, Mfaransa hajui kusoma Kiswahili. Hivyo, kutumia lugha mbili au zaidi itasaidia kwa sababu watumiaji wanaweza kusoma na kutambua maelezo ya bidhaa husika yanahusu nini kwa lugha waijuayo. Kwa kifupi, makampuni huandika maelezo ya bidhaa zao kwa lugha mchanganyiko ili kufanikisha biashara zao ziweze kuendelea... **Chanzo: Uwandani (2021)**

Maelezo ya mtoataarifa hapo juu yanaonesha umuhimu wa kutumia lugha zaidi ya moja kwa ajili ya kuongeza fursa ya mawasiliano na biashara kwa wadau wa kilimo. Maelezo haya yana maana kwamba matumizi ya lugha zaidi ya moja yanasaidia hadhira yenye usuli changamani wa lugha. Hivyo, kampuni zinatumia mbinu ya kuandika lugha zaidi ya moja kwa nia ya kuifikishia jamii huduma kwa urahisi yaani, kila mteja anafikiwa na kuhudumiwa kwa lugha anayoifahamu. Kwa jumla, juhudi za kufikisha taarifa za biashara kwa wateja ambao wana usuli wa lugha tofauti na ya mzalishaji unahitaji matumizi ya lugha kimkakati ili kuvutia wateja.

Uchambuzi uliofanyika kuhusiana na matumizi ya lugha katika maduka ya pembejeo za kilimo umebaini kuwapo kwa ukinzani wa lugha. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mawasiliano baina ya wahudumu wa maduka hayo na wakulima yametawaliwa na Kiswahili. Kwa upande mwingine, maandishi yanayoeleza na kunadi bidhaa za kilimo zinazouzwa madukani yametawaliwa na lugha ya Kiingereza. Hivyo basi, hakuna uwiano baina ya lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi. Kimsingi, ukinzani huu unasababishwa na suala la kutokufanya maamuzi kuhusu matumizi ya lugha katika sekta ya kilimo, jambo ambalo haliafikiani na Nadharia ya Ufanyaji Uamuzi.

Matumizi ya Lugha katika Taasisi za Mafunzo ya Kilimo

Elimu ya kuanzia ngazi ya sekondari na mafunzo mengine yanayotolewa kwa watu waliohitimu masomo ya sekondari na kuendelea yanapaswa kutolewa kwa Kiingereza (WEMU, 2014). Hii ina maana kwamba katika mafunzo ya kilimo lugha iliyopendekezwa ni Kiingereza. Kimsingi, hili ni eneo pekee katika sekta ya kilimo lililowekewa miongozo bayana kuhusu matumizi ya lugha. Hivyo, wataalamu wanaoendesha mafunzo na ushauri kwa wakulima na wafugaji nchini Tanzania huwa wanafundishwa kwa Kiingereza kutokana na sera ya lugha ya elimu iliyopo. Isitoshe, nchini Tanzania matumizi ya Kiingereza katika sekta ya mafunzo yanachangiwa na mtazamo kuwa lugha hiyo inahusika na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kwa mfano, mtoataarifa ambaye ni mwanafunzi wa SUA anakiri kuwa Kiingereza ni lugha ya sayansi na teknolojia kwa kusema:

...matumizi ya Kiingereza katika mfumo wa elimu ya kilimo kwa kiasi kikubwa yanachangiwa na kuwa hii ndiyo lugha inayobeba dhana mbalimbali za sayansi na teknolojia. Unajua Kiingereza katika masuala ya kitaalamu kama haya ya kilimo hakiwezi kuepukika kwa kuwa ndiyo lugha ya sayansi na teknolojia ya dunia... **Chanzo:** Uwandani (2021).

Maelezo hayo yanaonesha matumizi ya Kiingereza ni suala ambalo haliepukiki katika kutoa huduma za jamii (zikiwemo huduma za kilimo) kwa sababu lugha hii imepewa hadhi ya juu na wanajamii ulimwenguni. Kwa ujumla, muktadha wa mafunzo ya kilimo ni eneo pekee katika sekta ya utoaji wa huduma za kilimo linalokidhi matakwa ya Nadharia ya Ufanyaji Uamuzi (Carol Eastman, 1983). Katika eneo hili, uamuzi kuhusu uteuzi wa lugha ya kutolea mafunzo ya kilimo umefanyika kwa kuzingatia mhimili wa kuteua lugha miongoni mwa lugha zilizopo katika jamiilugha husika. Kwa hiyo, lugha ya Kiingereza katika mafunzo ya kilimo imeteuliwa kutoka miongoni mwa lugha za Tanzania, zikiwamo Kiswahili na lugha za kijamii. Haya ni matokeo ya kuwapo kwa sera ya lugha ya elimu inayogusa pia eneo la matumizi ya lugha kwenye mafunzo ya kilimo.

Hitimisho

Hali ya matumizi ya lugha katika utoaji wa huduma za kilimo ni ya wingilugha. Lugha zilizodhihirika kutumiwa katika eneo la utafiti ni Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa, Kihispaniola na Lugha za Kijamii. Hata hivyo, lugha hizo hazina uamilifu unaolingana kimatumizi, zipo lugha zilizotumiwa kwa kiwango cha juu na nyingine zimetumiwa kwa kiwango cha chini kabisa. Utafiti huu umehitimisha kuwa matumizi ya Kiingereza na Kiswahili ni ya kiwango cha juu zaidi kuliko lugha nyingine. Mazungumzo ya wadau wa kilimo yanatawaliwa na Kiswahili ilhali maandishi yanatawaliwa na Kiingereza. Lugha zingine kama vile Kifaransa na Kihispaniola nazo zimebainika kutumiwa ingawa kwa kiwango cha chini. Hali hii inatokana na lugha hizo kutokuwa na uamilifu mkubwa kimatumizi nchini Tanzania. Isitoshe, lugha hizi kila zilivyotumika zimekuwa zikiambatanishwa na Kiingereza. Kwa kifupi, matumizi ya lugha hizo aghalabu hudokeza nchi mtengenezaji wa bidhaa husika. Nazo lugha za Kijamii zimetumiwa kwa kiwango cha chini kwani zinatumiwa na makundi ya jamii ndogondogo zinazounda jamii moja pana ya Watanzania. Matumizi ya lugha hizi yanalenga kuziba pengo la kimawasiliano hasa kwa wasiojua vyema Kiswahili. Kwa ujumla tofauti hizi za kimatumizi zinatokana na kukosekana kwa sera ya lugha katika utoaji wa huduma za kilimo ambayo ingeweza kudhibiti matumizi kama haya.

Marejeo

- Batibo, H. (1992). *The Fate of Ethnic Languages in Tanzania*. Katika B. Mathias (Mh.), *Language Death: Factual and Theoretical Explorations with Special Reference to East Africa* (kur. 85–98). Mouton de Gruyter.
- Brock-Utne, B. (2000). *Whose Education for All? Recolonization of the African Mind*. Falmer Press.
- Eastman, C. M. (1983). *Language Planning: An Introduction*. Chandler & Sharp Publishers, Inc.
- Hans, M. M. (2017). Tathmini ya Utekelezaji wa Matamko ya Viongozi Waandamizi wa Serikali ya Tanzania kuhusu Matumizi ya Kiswahili. Katika Jilala, H. (Mh.), *Nadbaria ya Tafsiri, Ukalimani na Undaji wa Istilabi* (kur. 447–496). Daud Publishing Company Limited.
- Kaplan, R. B., & Baldauf, R. B. (1997). *Language Planning: From Practice to Theory*. Multilingual Matters.
- Kawonga, G. (2020). "Nafasi ya Lugha ya Kiswahili katika Mandhari Lugha ya Jiji la Mbeya Nchini Tanzania". *Tasnifu ya Uzamivu* (Haijchapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kidami, R. P. (2017). 'Matumizi ya Lugha katika Mandhari-Lugha ya Jiji la Dar es Salaam: Ulinganishi wa Dhima za Kiswahili na Kiingereza'. *JULACE: Journal of University of Namibia Language Centre*, 2(1), 134–157.
- Lusekelo, A., & Alphonse, C. (2018). The Linguistic Landscape of Urban Tanzania: An Account of the Language of Billboards and Shop-Signs in Districts. *Journal of Language, Technology and Entrepreneurship in Africa*, 1–28.

- Mary, L. K. (2015). Language and the Development of Agriculture in Kenya. *Research on Humanities and Social Sciences*, 5(2), 27–34.
- Massamba, D. P. B. (2007). *Kiswahili Origins and The Bantu Divergence Convergence Theory: Institute of Kiswahili Studies*. TUKI.
- Matalu, K. (2013). "Challenges of Using English Language in the Tanzanian Agricultural Sector: A Case of Maswa and Bariadi Districts". *Tasnifu ya Umahiri*. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachpishwa).
- Mekacha, D. K. . (2011). *Isimujamii: Nadbaria na Muktabha wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- MLUTA. (2009). *Atlasi ya Lugha za Tanzania*. Mradi wa Lugha za Tanzania.
- Msanjila, Y. P. (2009). Haja ya kuwa na Sera Toshelevu ya Lugha Tanzania:Uzoefu na Changamoto. *Mulika*, 28(1), 61–72.
- Msanjila, Y. P., Y.M.Kihore, & D.P.B.Massamba. (2011). *Isimujamii: Sekondari na Vyuo*. TUKI.
- Ngowa, N. J., & Ryanga, S. (2011). Kiswahili na Usalama wa Chakula: Vikwazo vya Lugha. *Kioo Cha Lugha*, 9(1), 59–72.
- Oladele, O. I. (2006). Multilinguality of Farm Broadcast and Agricultural Information Access in Nigeria. *Nordic Journal of African Studies*, 15(2), 199–205.
- Roy-Campbell, Z., & Qorro, M. (1997). *The Language Crisis in Tanzania: The Myth of English Versus Education*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Rubin, J., & Jernudd, B. . (1971). *Can Languages Be Planned? Sociolinguistic Theory and Practice for Developing Nations*. University Press of Hawaii.
- Rugemalira, J. (2013). Language Policy and Planning – the Tanzania Experience. Katika P. Akumbu & B. Chiatoh (Wah.), *Language Policy in Africa: Perspectives for Cameroon*. Miraclaire Publishing.
- Shohamy, E. (2006). *Language Policy: Hidden Agenda and New Approaches*. Routledge.
- Spolsky, B. (2012). *The Cambridge Handbook of Language Policy*. Cambridge University Press.
- Sylvester, J. (2011). "Ubadilishaji Msimbo Bungeni na Athari Zake kwa Wasikilizaji". *Tasnifu ya Umahiri* (Haijachpishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Thornburn, T. (1971). Cost-Benefit Analysis in language planning. Katika Joan Rubin & B. H. Jernudd (Wah.), *Can language be planned?* (kur. 253 – 262). University of Hawaii Press.
- TUKI. (2000). *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- URT. (2017a). *Agricultural Sector Development Programme Phase II (ASDP II)*. The United Republic of Tanzania.
- URT. (2017b). *Annual Agriculture Sample Survey Crop and Livestock Report*.
- WEMU. (2014). *Sera ya Elimu na Mafunzo*. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.
- WEU. (1997). *Sera ya Utamaduni*. Wizara ya Elimu na Utamaduni.
- Yuming, L. (2015). *Language Planning in China* (Juz. 4). Walter de Gruyter.